


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Barabara ya  
Kilimatinde Cheyo,  
S.L.P. 1020,  
45112  
TABORA,  
Barua Pepe: [rbctabora@pccb.go.tz](mailto:rbctabora@pccb.go.tz).  
TANZANIA.  
[www.pccb.go.tz](http://www.pccb.go.tz)

---

**TAARIFA KWA UMMA**

---

**TABORA, 07 DESEMBA 2020**

**RUSHWA KWENYE POS KUMFIKISHA MHASIBU WA MAPATO  
MANISPAA YA TABORA MAHAKAMANI**

TAKUKURU Mkoa wa Tabora kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwendesha Mashtaka wa Serikali Mkoa wa Tabora mnamo tarehe 07 Desemba 2020 inatarajia kumfikisha Mahakamani SYLVESTER BULUGU MICHAEL Mhasibu wa Mapato wa Halmashauri ya Manispaa ya Tabora kwa makosa matatu ya rushwa.

Makosa hayo yalifanyika kati ya mwezi Machi 2018 na Juni 2019. Sylvester Bulugu Michael akiwa Mhasibu wa Manispaa ya Tabora na akiwa na jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato Manispaa ya Tabora kutoka vyanzo mbalimbali na kuziwasilisha fedha hizo benki, alijihusisha na vitendo vya rushwa.

Uchunguzi uliofanywa na TAKUKURU mkoa wa Tabora ulithibitisha kwamba mnamo tarehe 28/02/2018 Sylvester Bulugu Michael aliandika barua kwenda kwa Afisa Tehama Manispaa ya Tabora na kuomba POS Mashine ili

kuingizia mapato yanayokuwa yanakusanywa katika chanzo cha Ofisi kuu ya Manispaa.

Kati ya mwezi Machi 2018 hadi Juni 2019 POS mashine aliyokabidhiwa Sylvester Bulugu Michael ilikusanya mapato ya jumla ya Sh. 19,648,175 kutoka vyanzo mbalimbali. Mtuhumiwa katika taarifa ya makusanyo ya fedha aliyoiandaa kwa kipindi cha kuanzia Machi 2018 hadi Juni 2019 alionesha kwamba amekusanya kiasi cha Sh. 19,648,175 na kudai kwamba kiasi hicho kilichokusanywa kiliingizwa benki katika akaunti ya Manispaa ya Tabora "*OWN SOURCE COLLECTION*" lakini uchunguzi umebaini kuwa taarifa haikuwa ya kweli kwani kiasi cha **Sh. 5,356,000** hakikuingizwa benki kama ilivyooneshwa kwenye taarifa.

Hivyo leo tarehe 07 Desemba 2020 Sylvester Bulugu Michael atafikishwa Mahakamani kwa makosa matatu ya matumizi mabaya ya mamlaka kinyume na kifungu cha 31, ufujaji na ubadhirifu kinyume na kifungu cha 28 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007 pamoja na Kuisababishia Serikali hasara kinyume na Aya ya 10 ya jedwali la kwanza ikisomwa pamoja na vifungu vya 57 (1) na 60 (2) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi sura ya 200 toleo la mwaka 2019.

**KATIKA HATUA NYINGINE** TAKUKURU Mkoa wa Tabora leo tarehe 07 Desemba 2020 inamrejeshea Mwalimu VERONICA JOSEPH fedha kiasi cha **Sh. 6,000,000/=** kati ya **Sh 10.000,000/=** alizokuwa anadai baada ya kudhulumiwa na Mhe. YUSUPH KITUMBO Diwani wa Kata ya Cheyo ambaye alimuuzia gari na baadaye kulichukua gari hilo alilomuuzia kwa madai kuwa angemrudishia. Licha ya Mwalimu Veronica Joseph kudai arudishiwe gari au fedha zake tangu mwezi Juni 2019 YUSUPH KITUMBO hakurudisha fedha wala gari hadi TAKUKURU mkoa wa Tabora ilipoingilia kati na kumtaka aanze kurejesha fedha anazodaiwa.

Aidha, TAKUKURU mkoa wa Tabora leo inarejesha kiasi cha **Sh. 9,507,000/=** kwa walimu watatu ikiwa ni fedha zilizookolewa kutoka


mikononi mwa Kampuni ya Misana Michael Mtaturu, Marco Maduka na Kija Dotto wanaokopesha mikopo kinyume na taratibu. Walimu wanaorejeshewa fedha ni Sophia Mathew, Anna Mtaturu na Regina Mponeja

Vilevile leo tunarejesha **Sh.1,546,000/=** kwa Boniface Daniel ambaye alikuwa kibarua TTCL baada ya kufanya kazi na kutolipwa haki yake na mtumishi wa TTCL aliyekuwa akiwasimamia Bw. Benedict Kiagho. Fedha hizi zinarejeshwa baada ya kufanya uchunguzi na kujiridhisha kuwa Boniface Daniel alifanya kazi ya kusafisha na kukata pori kwa ajili ya kuchimba mtaro wa kutandaza nyaya za mawasiliano ya simu lakini hakupewa malipo aliyostahili kwani sahihi yake ilighushiwa.

Napenda kuwashukuru sana waandishi wa habari kwa namna mnavyohabarisha umma kuhusu madhara ya rushwa ndani ya mkoa wetu wa Tabora. Asanteni sana.

Aidha nawashukuru wananchi wa mkoa wa Tabora kwa ushirikiano mnaotoa kwa TAKUKURU. Tunawaomba muendeleo kutoa tarifa ya vitendo vya rushwa kupitia namba 113 au TAKUKURU APP nasi tunaahidi kuzifanyia kazi kwa weledi mkubwa. Pia kuna miradi ya maendeleo inayoendelea katika maeneo yenu ikiwa kuna vitendo vya Rushwa vitakavyojitokeza katika miradi hiyo msisite kutoa taarifa nasi tunaahidi kuzifanyia kazi.

Asante



Musa Chaulo

**MKUU WA TAKUKURU MKOA**